

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



ZABUNI NAMBA: LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/24, LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/25 & LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/26

TANGAZO LA ZABUNI

UWAKALA WA UKUSANYAJI USHURU KATIKA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inakusudia kuweka mawakala kwa ajili ya **uwakala wa ukusanyaji ushuru katika Halmashauri Manispaa ya Kinondoni**

1. Halmashauri ya Manispaa ya kinondoni inawakaribisha kuleta Zabuni zenu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II
2. Wazabuni wenye nia ya kufanya kazi za uwakala **wa ukusanyaji** Ushuru wanaweza kukagua nyaraka za zabuni na kupata maelezo kutoka kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni S.L.P.31902 Dar es salaam siku ya Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za Sikukuu za Kitaifa kuanzia saa mbili hadi saa tisa na nusu jioni. Kwa zabuni zifuatazo;
 - i. **Zabuni ya Uwakala wa ukusanyaji ushuru wa maegesho ya bajaji na pikipiki katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yenye namba LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/24**
 - ii. **Zabuni uwakala wa ukusanyaji ushuru wa samaki, mazao mengine ya uvuvi na maegesho ya vyombo vya uvuvi na usafiri wa majini katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yenye namba LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/25**
 - iii. **Zabuni ya Uwakala wa ukusanyaji ushuru wa Vyoo katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni yenye namba LGA/017/HQ/2017 – 18/NCS/26**
3. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa kuleta barua ya maombi na malipo ya fedha taslimu yasiyorudishwa (Non – refundable) ya **shilingi elfu hamsini tu (50,000.00)** gharama hizo ni kwa **kila “Lot”** kwa zabuni husika kwa Mkurugenzi wa Manispaa S.L.P. 31902 Kinondoni.

Zabuni zote ziwe na nakala halisi (original) moja (1) na nakala kivuli mbili (2) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na

maandishi juu na kuandikwa jina la zabuni, namba ya zabuni na Lot yake husika yaani
“Zabuni ya uwakala wa ukusanyaji ushuru wa
.....yenye Zabuni Na. LGA/017/HQ/2017 –
18/NCS/24, 25 au 26 LOT No.

4. Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa anuani ifuatayo:-
**Mkurugenzi wa Halmashauri,
Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,
S.L.P 31902
Dar Es Salaam.**
5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ni **tarehe 15 Disemba, 2017 saa (04.00) nne kamili asubuhi**. Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu, mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa Manispaa.
6. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji Zabuni, kwa hali yoyote ile Zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Aron T. Kagurumjuli
**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI**